



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA
MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU



Unapojuibu tafadhali taja:

Kumb. Na. UDC/E.50/04/07

11 Februari 2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu anawatangazia nafasi za kazi watanzania wote wenye sifa za kuajiriwa katika nafasi ya Mtendaji wa Kijiji Daraja la III. Hii ni kutokana na Kibali cha Ajira Mbadala Kilichotolewa kwa barua yenyewe Kumb. Na. FA.170/376/01 "B"/112 ya tarehe 10 Januari 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

A. MTENDAJI WA KIJJI DARAJA III – Nafasi 02.

SIFA ZA MWOMBAJI.

1. Awe amehitimu Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI).
2. Awe amehitimu mafunzo katika ngazi ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo; Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii, na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI/ MAJUKUMU.

1. Atakuwa Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji;
2. Atakuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji;
3. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji;
4. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji, na Kiongozi wa Wataalamu waliopo katika kijiji.
5. Kutasfiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu za Serikali katika kijiji.
6. Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali;
7. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji;
8. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji;
9. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji na
10. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.
11. Kusimamia Mapato na Matumizi ya Halmashauri ya Kijiji.

Mshahara: Ngazi ya Mshahara wa Serikali (**TGS B**).

Masharti ya Kazi: Ajira ya Kudumu na Pensheni.

VIGEZO NA MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI.

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania na umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18.
2. Mwombaji awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote la jinai.
3. Waombaji wote waambatanishe nakala za vyeti vya taaluma, nakala ya cheti cha Kidato cha nne, na sita vilivyothibitishwa na Hakimu au Wakili anayetambulika na Serikali.
4. Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa iliyothibitishwa na Hakimu au Wakili anayetambulika na Serikali.
5. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed Curriculum Vitae) ikiwa na anuani, namba za simu za kuaminika, pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu (3) na picha moja ya "passport size" ya hivi karibuni (iandikwe majina kwa nyuma).
6. Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, Hati za matokeo za kidato cha nne na sita (Form IV and VI Results Slips) na Transcript ambayo haikuambatanishwa na cheti havitakubaliwa.
7. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vinahakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (NECTA au NACTE).
8. Waombaji ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe nafasi hizi.
9. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma kwa sababu yoyote ile hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi.
10. Waombaji watakaowasilisha vyeti, na taarifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria na mamlaka zinazohusika.
11. Maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
12. Kwa waombaji wenye vyeti vya ngazi yaani NTA Level 4 (Basic Technician Certificate), na NTA Level 6, maombi yao hayatafanyiwa kazi.
13. Waombaji wote waambatanishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA), au Namba ya Utambulisho wa Uraia (National Identification Number) kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
14. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni siku ya Alhamisi, tarehe 30 Machi 2023, saa 09:30 Alasiri.**
15. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu,
S.L.P. 50,
KAHAMA.



Deus Kakulima

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI





Nakala:
Katibu Tawala (M),
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S.L.P 320,
SHINYANGA.

Katibu Tawala (W),
Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,
S.L.P 01,
KAHAMA.

Mbao zote za Matangazo,
Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Msalala, na Manispaa ya Kahama.
KAHAMA.

Tovuti ya Halmashauri: www.ushetudc.go.tz